**JESMA 008**

# JARIBIO LA NANE K.C.P.E
## DARASA LA NANE 2022

**KISWAHILI SEHEMU YA KWANZA: LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

### SOMA KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibu. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.
3. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala si katika kijitabu hiki cha maswali.

### JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

4. Tumia penseli ya kawaida.
5. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

6. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule. Na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
7. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
8. Iweke safi karatasi yako ya majibu.
9. Kwa kila swali 1 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C na D. Ni jibu **MOJA** tu kati ya hayo manne ambayo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
10. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**11.** Andika wingi wa sentensi ifuatayo.

Mswaki uliotumiwa na kijana ulikuwa safi.

A. Miswaki zilizotumiwa na vijana zilikuwa safi.
B. Miswaki uliotumiwa na vijana ulikuwa safi.
C. Miswaki iliyotumiwa na vijana ilikuwa safi.
D. Miswaki iliyotumiwa na vijana ilikuwa misafi.

Jibu sahihi ni C

[1] [A] [B] [C] [D]   [11] [A] [B] ▬ [D]   [21] [A] [B] [C] [D]   [31] [A] [B] [C] [D]   [41] [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 11, kisanduku chenye herufi C ndicho kilichochorwa kistari.

11. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
12. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kitabu hiki cha maswali kina kurasa 8 zilizopigwa chapa**

**Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa ma li yote yamo.**

Tovuti: www.jesmapublishersltd.com Barua pepe: jesmapublisher on.com

 © Jesma Publishers & Educational Booksellers [illegible] **GEUZA UKURASA**

JESMA JARIBIO LA NANE 2022 008

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi | **Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* **1** *mpaka* **15.** *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.*

Ni jambo muhimu kwa kila mja __1__ malengo maishani. Mtu __2__ kiholela __3__ azma yoyote, huwa sawa na chombo kinachoendeshwa bila mwelekeo maalum. Mwanafunzi naye, kwa kujiwekea malengo yake __4__ hulivua joho la ajizi na kuwa na __5__ ya kufanikiwa sio tu kielimu __6__ maishani __7__. Hata hivyo, ni lazima tuelewe kuwa malengo pasipo uwajibikaji si chochote si lolote. Ufanisi unahitaji bidii kwa kuwa __8__.

**1.** A. kuyawekea B. kumwekea C. kujiwekea D. kuiweka.

**2.** A. angeishi B. anapoishi C. anaoishi D. akaishi

**3.** A. licha ya B. fauka ya C. dhidi ya D. minghairi ya

**4.** A. , B. ; C. : D. -

**5.** A. ari B. shauku C. ghamidha D. lengo

**6.** A. mbali na B. kwani pia C. japo pia D. bali pia

**7.** A. yake B. pake C. mwake D. kwake

**8.** A. imara ya jembe kaingoje shambani B. mtaka cha mvunguni sharti ainame
C. tone na tone huwa mchirizi D. Dunia zikiwa pamoja kilicho mbali huja.

Majadiliano yalikuwa __9__ huku wanafunzi __10__ hoja zao kwa hamu. Mjadala __11__ haki za watoto. __12__ ya haki zilizotajwa ni elimu, afya, mavazi na lishe bora __13__ kukua vizuri. Isitoshe, ilionekana ni muhimu kwa mtoto kupewa huduma maalum __14__ naye __15__ kwa kutunza rasilimali zilizopo.

**9.** A. yamepamba moto B. yamepiga mbiu C. yameshika tamu D. yamepiga chuku

**10.** A. wamejadili B. walijadili C. wakijadili D. waliojadili

**11.** A. yenyewe ilihusu B. wenyewe ulihusu C. wenyewe ilihusu D. yenyewe ulihusu

**12.** A. Kati ya B. Mithili ya C. Kando na D. Baadhi ya

**13.** A. itakayomwezesha B. litakalomwezesha
C. kitakachomwezesha D. utakaomwezesha

**14.** A. angaa B. aghalabu C. almradi D. ilhali

**15.** A. awajibishe B. awajibike C. awajibiwe D. awajibie



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.*

**16.** Tambulisha matumizi ya **na** katika sentensi ifuatayo.
Napenda kujifunza kwa tarakilishi za kisasa.
A. Kuonyesha wakati uliopo.
B. Kuonyesha mnyambuliko wa kitenzi.
C. Kuonyesha nafsi ya kwanza.
D. Kuonyesa ufupisho wa nafsi.

**17.** Chagua usemi halisi wa sentensi ifuatayo.
Baba aliwaambia wanawe kuwa wangeenda shuleni siku ambayo ingefuata.
A. "Tunaenda shuleni kesho," baba aliwaambia wanawe.
B. "Siku ifuatayo wangeenda shuleni," baba waliwaambia wanawe.
C. "Tutaenda shuleni kesho," baba na wanawe waliambiwa.
D. "Kesho mtaenda shuleni," baba aliwaambia wanawe.

**18.** Kipi ni kitenzi kilichoundwa kutokana na sifa?
A. Ulevi - lewa
B. Mwaminifu - uaminifu
C. Ucheshi - mcheshi
D. Mchafu - chafua

**19.** Maneno yaliyopigiwa mistari katika sentensi ifuatayo ni,
Dalali alikuwa ameshika vitu vichache mkononi.
A. kiwakilishi, kielezi
B. kivumishi, kielezi
C. kivumishi, kiwakilishi
D. kivumishi, kihusishi

**20.** ________ ni kwa shambani, kichanja ni kwa jikoni.
A. Kwanja
B. Kekee
C. Singe
D. Kifumbu

**21.** Upi ni ukanusho sahihi wa sentensi.
Kijana aliyekuwa hapa anapenda muziki.
A. Kijana asiyekuwa hapa hapendi muziki.
B. Kijana ambaye hakuwa hapa anapenda muziki.
C. Kijana aliyekuwa hapa hapendi muziki.
D. Kijana hakuwa hapa wala hapendi muziki.

**22.** Tegua kitendawili.
Bi kikongwe apepeta ufuta.
A. mtama
B. kope
C. mvi
D. upepo

**23.** Ni maelezo yapi **yasiyo** sahihi.
A. Kumba ni kumsukuma mtu kwa bega.
B. Kumba ni hali ya kumlaghai mtu.
C. Kumba ni samaki jamii ya perege.
D. Kumba ni jambo linaloathiri watu wengi.

**24.** Beberu ni kwa mbarika kama ilivyo fahali kwa
A. ng'ombe
B. mtamba
C. tembe
D. nzao

**25.** Andika umoja wa sentensi.
Nywele zenu ndefu ziliwavutia.
A. Unywele wako mrefu ulikuvutia.
B. Nywele yako ndefu ilikuvutia.
C. Unywele wake mrefu ulimvutia.
D. Nywele yenu ndefu ilikuvutia.

**26.** Ni methali gani iliyo na maana tofauti na nyingine?
A. Papo kwa hapo kamba hukata jiwe.
B. Usiache mbachao kwa msala upitao.
C. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.
D. Mtumai cha ndugu hufa maskini.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

27. Nomino siagi, samli na mvua huorodheshwa katika ngeli gani?

A. I - ZI
B. U - ZI
C. I - I
D. LI - YA

28. Panga vifungu vifuatavyo kuunda sentensi sahihi.

*(i) angekuja siku gani*
*(ii) angenitembelea*
*(iii) hakuniarifu kuwa*
*(iv) wala sikujua*
*(v) nyumbani kwangu*

A. (ii), (v), (iv), (i), (iii)
B. (v), (iii), (ii), (iv), (i)
C. (iii), (ii), (iv), (v), (i)
D. (iii), (ii), (v), (iv), (i)

29. Sehemu ya bei ya kitu inayotolewa mwanzoni ili kukifungia kusinunuliwe na mwingine ni

A. arbuni
B. mtaji
C. koto
D. riba

30. Chagua sentensi iliyotumia kiingizi kifaacho

A. Wallahi! Wameahidi kunisaidia.
B. Ebo! Maoni yako yatanisaidia sana.
C. Alhamdulilah! Mama amepata nafuu.
D. Shabash! Nimefeli mtihani wa kitaifa.

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia* **31** *mpaka* **40**

Baada ya muda mrefu, nilikuja kukubaliana na wahenga kuwa hakuna marefu yasiyokuwa na ncha. Sayo alikuwa barobaro mmoja katika kitongoji chetu aliyezichoma nyoyo za wengi. Alikuwa na hulka ambazo hakuna aliyekubaliana nazo. Hali hii haikuchangiwa hata chembe na malezi aliyopewa na wavyele wake kwani hawakumwengaenga kama yai la mbuni wala kumlea kwa tunu na tamasha. Hali yao ya utashi na uhawinde isingewaruhusu. Walimlea mwana wao kwa kumwonyesha machungu yote ya dunia na kumwonyesha kuwa lazima jasho limdondoke ili mkono uende kinywani. Mara kwa mara, Bwana na Bi. Mwakazi walimwonya mwanao dhidi ya hulka zake benibeni lakini aliyeambiwa alikuwa kihongwe; alitia uta masikioni. Basi baada ya kuona kuwa mwanao aliyatia kapuni mawaidha yote, wavyele wa Sayo waliamua kutupa jongoo na mti wake. Waliamua kumwacha afunzwe na ulimwengu kwani mtoto akililia wembe mpe.

Sayo alizidisha maovu yake kote kitongojini na kila mara, majirani walilalamika juu yake. Aliiba mali ya wengine na kuyauza, aliongea na wakuu wake bila staha na aliwachokoza watoto wengine kijijini. Shuleni, masomo yalimlemea na baadaye akahamia mjini ambako maisha hayakumridhisha. Kazi kwake iliadimika kama kaburi la baniani na lishe ilikuwa nadra kupatikana. Basi ilibidi atafute njia ya kuzumbua riziki na akaonelea ni bora arefushe mkono. Huko kijijini, wakazi walijawa na bashasha alipoondoka kwani walikua na amani na utulivu.

Sayo hakuishi kwa muda mrefu mjini kabla ya tabia yake kugunduliwa na kuwekewa mtego wa kumkamatia. Polisi waliokuwa wakishika doria katika mtaa alioishi waligundua tabia yake na kuanza kumchunguza baada ya kudokezewa na wakazi kuwa Sayo alikuwa mwizi. Laiti angejua kuwa wenzake wangekufa kifo kibaya namna walivyokufa, basi angeiacha tabia yake ya wizi. Maonyo aliyopewa na watu waliomjali yaliangukia masikio yenye komango kwani Sayo alikuwa hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini.

Basi usiku mmoja, genge aliloenda nalo kuiba lilimwita waende wakatekeleze wajibu wao katika duka moja huko mtaani. Hawakujua kuwa hiyo ilikuwa siku yao ya arubaini. Basi wakati ziara yao ilipofika kileleni, walisikia milio ya risasi nje ya duka. Kila mmoja alitoka shoti, miguu niponye. Juhudi za kutoroka ziligeuka ngoma goya walifyatuliwa risasi wakaaga dunia wote ila Sayo ambaye alikuwa wa kwanza kutundika guu begani. Baadaye alijitokeza alipopata habari kwamba alikuwa akisakwa. Alihukumiwa kifungo cha mwongo mmoja gerezani na wakati alipoachiliwa huru, alikuwa ameiasi mienendo mbovu ya awali.

Alirejea kayani akawaomba radhi wavyele na wakazi wengine. Wale hawakuwa na budi kumwia radhi walipoona kuwa huyo hakuwa yule wa zamani bali mwingine alinyooka kama kondoo. Wavyele walimpa mtaji akaanzisha biashara ya kununua na kuuza mifugo kwani aligundua kuwa kazi mbi si mchezo mwema. Pia hakusahau kufungua kituo cha kuwafunza vijana kuhusu jinsi ya kujihusisha na miradi yenye manufaa kwao na kuachana na tabia kama vile usherati, uporaji na uraibu wa mihadarati. Kila mtu kijijini alifurahia mabadiliko aliyoyapata Sayo. Kwa hakika mui huwa mwema.

31. Kulingana ya aya ya kwanza,
A. malezi duni yalinifanya Sayo apotoke kimaadili.
B. hulka za Sayo zilikuwa kero kwa wakazi.
C. kufukuzwa shule kwa Sayo kuliathiri mienendo yake zaidi.
D. wavyele walipuuza wajibu wao katika malezi ya Sayo.

32. Ni dhahiri kuwa aila ya Sayo ilikuwa ya
A. walalahai
B. walalaheri
C. walalamishi
D. walalahoi.

33. Si kweli kusema kuwa Sayo,
A. alilelewa kwa vitanga vya mikono.
B. alihimizwa aweze kutia juhudi maishani.
C. alidekezwa na kuengwaengwa na wavyele.
D. alifunzwa umuhimu wa uadilifu maishani.

34. Maneno '<u>alikuwa kihongwe</u>' yametumia tamathali gani ya usemi?
A. tanakali
B. nahau.
C. kinaya.
D. sitiari.

35. Baada ya kuhamia mjini, Sayo aliendeleza hulka yake mbovu kwa kuwa,
A. alihitaji kukidhi mahitaji yake.
B. ajira haikuwa jambo nadra kwake.
C. alikuwa ameacha masomo kwa ukosefu wa karo.
D. alihitaji kukabiliana na utashi wa aila yake.

36. Zifuatazo ni sifa za Sayo **ila**,
A. mtukutu.
B. mkaidi.
C. msumbafu.
D. mkunjufu.

37. Uovu wa Sayo na genge lake ulikomeshwa kutokana na
A. uhusiano mwema baina ya polisi na wakazi.
B. taarifa alizotoa mwenye duka kwa polisi.
C. kuzidi kwa vitendo vya kikatili mtaani.
D. kutokuwa waangalifu wakitekeleza uhalifu.

38. Misemo ifuatayo ni kweli kuhusu Sayo isipokuwa
A. aliponea chupuchupu.
B. alitangulia mbele ya haki.
C. alitia masiko nta.
D. alitupa jongoo na mti wake.

39. Wavyele wa Sayo na wanakijiji wengine walimkumbali Sayo kwa kuwa,
A. wenzake waliangamia mkononi mwa polisi.
B. alifungwa gerezani na kukamilisha kifungo.
C. mienendo yake ilikuwa imechukua mkondo ufaao.
D. walikuwa wapenda amani waliopuuza mienendo ya wengine.

40. Ushauri aliowapa vijana hasa ulihusu,
A. kuasi mienendo hasi na kuanzisha biashara kubwa.
B. kuandama hulka bora na kushiriki shughuli zenye manufaa.
C. kuacha tabia za zamani na kuingiliana vyema na wanajamii.
D. kuwaheshimu wazazi na kupuuza mienendo ya wenzao.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

*Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali kuanzia nambari* **41** *mpaka* **50**

Mazingira ni mambo au hata hali ambazo hutuzunguka sisi. Binadamu huishi karibu na viumbe, vitu hali na hata watu wa kila aina. Aidha, miti, mito, maziwa, bahari na hata hewa tuipumuayo ni sehemu ya mazingira yetu. Majirani zetu wa karibu na wa mbali pia ni sehemu muhimu ya mazingira. Mazingira ni johari ni tunu tuliyotunukiwa na jalali na hatuna budi kuyadumisha la sivyo tutaathiri maisha yetu na ya vizazi vijavyo.

Mazingira yetu hutuneemesha kuwa njia maridhawa. Kwa mfano, miti humnufaisha binadamu kwa mengi licha ya kuwa baadhi yayo hutumika kama chakula, mingi pia hutumiwa kama pambo la mazingira. Tukikata miti kiholela, taifa letu litakumbwa na uhaba wa chakula ambao hautawaathiri wakazi kiafya tu lakini watakosa nguvu za kuendesha uchumi wa taifa.

Miti imetumiwa kwa muda mrefu kutupatia dawa za maradhi sugu yanayozivamia jamii zetu. Ni nani asiyeujua mti wa mwarubaini unaoaminika kutibu takriban ndwele arubaini? Miti pia hutumiwa kutengenezea baadhi ya nguo, kusafisha hewa, kutupa kivuli wakati wa kiangazi na kutukinga na miale mikali ya jua. Licha ya hayo, misitu ni makazi ya baadhi ya hayawani.

Uchafuzi wa mazingira ni miongoni mwa masuala ambayo yamewafikirisha wakazi wengi kwa miongo. Licha ya kuwa ustawi wa viwanda umeleta faida chungu nzima, ustawi uu huu umeleta athari za kimazingira. Mawingu ya moshi yanayotoka viwandani hayatishi tu afya zetu bali huyafanya mazingira kutopendeza. Moshi uingiapo katika mapafu yetu huyachoma na kusababisha magonjwa kama pumu na saratani ya mapafu.

Baadhi ya viwanda vinavyotengeneza dawa na kemikali mbalimbali huigeuza mito na maziwa yetu kuwa majaa ya kurundika taka zao. Kitendo hiki huwaua wanyama wa baharini kama vile samaki. Isitoshe, mafuta yanayovuja kutoka vyombo vya baharini huendelea na maangamizi ya viumbe hao.

Ustaarabu wa kigeni ulipomfikia mwafrika aligundua umuhimu wa kupika chakula akaanza kukata miti ili apate kuni na makaa. Maendeleo haya pia yalimwonyesha haja ya kutoishi mwituni, akakata miti kujengea nyumba, kuundia samani na kupata maeneo ya kulima. Hali hii iliendelea kwa muda mrefu kabla ya kutanabahi kuwa mazingira yalikuwa hatarini. Ikawa viongozi wanatoa wito "ukikata mti mmoja panda mingine miwili".

Wanyama wa porini nao wamo hatarini. Kulizuka kundi la watu waliojali maslahi yao tu. Kwa kutawaliwa na ubinafsi, waja hawa walianza kuwawinda wanyama na kuwaangamiza. Ndovu waliwindwa kwa mabori nao vifaru wakaangamizwa kwa biashara ya vipusa. Duma na chui nao wakaangushwa kwa ngozi zao. Hali hii inatishia kutokomeza rasilimali hii muhimu.

Maendeleo katika sekta ya kilimo pia huchangia katika uchafuzi wa mazingira. Kemikali ambazo hupuliziwa wadudu na vimelea vingine huua viumbe wanaoishi kwenye udongo. Jambo hili huathiri uzalishaji wa mazao kwa namna moja au nyingine.

Ni kweli kuwa binadamu hufurahia mazingira mema. Hata hivyo ni jambo la kusikitisha kuona kuwa watu wasiojali maslahi ya wengine huwadhulumu kwa kuwaharibia mazingira. Kelele za magari mabovu huzidisha udhia. Uchezaji muziki kwa sauti ya juu hutatiza masikio na kuyadhuru. Lazima tujikumbushe kuwa ikiwa shughuli zote hizi za kimaendeleo zitafanywa bila tahadhari, basi tutabakia kutia vyanda midomoni na kusema, 'Tungalijua! mazingira sharti yahifadhiwe kwa vyovyote vile'.



Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi **| Mob: 0734579299**
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

41. Mazingira ni nini?
A. Vitu vinavyozunguka karibu na makao ya binadamu.
B. Chochote chenye manufaa kinachopatikana bila gharama.
C. Sehemu yoyote anayokaa binadamu na viumbe.
D. Viumbe, vitu na hali zinazomzunguka binadamu pale aishipo.

42. Mazingira ni johari; ndiko kusema,
A. yana thamani kubwa.
B. ni kitu adimu sana.
C. yana manufaa kichele.
D. mazingira ni uhai.

43. Yapi **si** kati ya manufaa ya miti kwa mujibu wa makala haya?
A. kuwasitiri viumbe.
B. tiba ya maradhi.
C. uhaba wa chakula.
D. kurembesha mazingira.

44. Mti unaojulikana kama mwarubaini,
A. huaminika kutibu magonjwa zaidi ya arubaini.
B. huaminika kutibu magonjwa karibu arubaini.
C. kwa hakika hutibu maradhi kama arubaini.
D. uliwahi kutibu magonjwa takriban arubaini.

45. Licha ya kuwa ustawi wa viwanda umeleta faida chungu nzima, ustawi uu huu umeleta athari za kimazingira. Chagua methali inayoambatana na kauli hii.
A. Baniani mbaya kiatu chake dawa.
B. Majuto ni mjukuu baadaye huja kinyume.
C. Hapana msiba usiokuwa na mwenziwe.
D. Hakuna bamvua lisilokuwa na usubi.

46. Pumu na saratani ya mapafu huchangiwa na,
A. kemikali zenye sumu.
B. uchafuzi wa hewa.
C. kutozingatia lishe bora.
D. mahusiano ya kiholela.

47. Ustaarabu unahusianaje na uharibifu wa kimazingira?
A. Haja ya kuishi vizuri ilichangia ukataji wa miti.
B. Kuondoka misituni kuliifanya miti kutelekezwa.
C. Umuhimu wa kapata tiba ulifanya miti ikatwe kupata dawa.
D. Vifaa vingi vya kiteknolojia viliundwa kwa malighafi ya miti

48. Kichocheo kikuu zaidi kwa uharibifu wa mazingira kulingana na kifungu ni
A. makazi na kuni.
B. ukosefu wa mali.
C. tamaa na ubinafsi.
D. kukosa maarifa.

49. Kulingana na aya ya mwisho,
A. uharibifu wa mazingira ni ukiukaji wa haki za binadamu.
B. Kelele za magari huchangia uchafuzi wa hewa.
C. Maendeleo yoyote yana athari nyingi kuliko faida.
D. Tukiwa na tahadhari tutaimarisha uharibifu wa mazingira.

50. Maana ya kutia vyanda midomoni ni
A. kuhangaika
B. kujuta.
C. kukasirika.
D. kuaibika.